# LEARNING BY EAR

## “Mizozo na utatuzi-palipo na wazee”

## Episode 8: “Uhaini dhidi ya binadamu”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters by scenes:**

**<u>SCENE ONE: MITUMBA SHOT OUTSIDE HIS HOUSE</u>**

- **Mitumba (m, 50)**
- **Lela (f, 20)**
- **Shani (f, 17)**
- **Masambo (m, 50)**
- **Gulu (m, 17)**

**<u>SCENE TWO: TORUBE ATTACK KIMBEBE IN THEIR TERRITORY</u>**

- **Lawi (m, 21)**
- **Several men shouting (at least 5)**
- **women wailing and children crying**

**<u>SCENE THREE: MATONGE, SOMBA AND KERO MEET</u>**

- **Matonge (m, 65)**
- **Somba (m, 55)**

- **Kero (f, 55)**

**Msimulizi**

**<u>INTRO:</u>**

Salamu kwako, popote ulipo, na karibu katika kipindi cha redio ukipendacho, Noa bongo! Jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha nane kadika hadithi ya, “**Palipo na wazee”.** Katika kipindi kilichopita, mkuu wa upelelezi Kero alisambaza bunduki kwa kila familia ya watorube, ili kuleta ugomvi na vita kati ya watorube na wakimbebe. Vita vya wenyewe kwa wenyewe vingelingelimpa fursa Rais Matonge kushinda tena uchaguzi. Wakati watorube wakijifunza kufyatua bunduki, Mitumba alipigwa risasi, alipotaka kutoka nyumbani kwake. Haya yalitokea baada ya mapatanisho ya shida kati ya watorube na wakoroma. Ni lipi litakalotokea? Je, Mitumba alipigwa risasi kwa bahati mbaya? Au kwa kusudi? Wacha tuchunguze, katika kipindi cha leo, **“ Uhalifu dhidi ya binadamu”.** Tunaanza, pale tulipoachia, Mitumba alipopigiwa risasi.

**SCENE ONE: MITUMBA SHOT OUTSIDE HIS HOUSE**

1. **MITUMBA:** **(still in pain)** Lelaaa! Shaniiii! Aaaaah nafaaa!!!!!!..

2. **LELA:** Baba, hautakufa. Ni mkwaruzo kidogo begani, nitaishughulikia. Utapona. **(rushing into the house)**

3. **SHANI:** **(sigh of relief)** Nashukuru Mungu! Nilifikiria utafariki baba. Nilikuwa nishaogopa.

4. **MITUMBA:** **(now relaxed)** Wasema polepole? Nilijuwa nimekwisha nilipopigwa risasi.

5. **LELA:** Pole baba, lakini ni lazima tukiweke kidonda dawa ndio kisivunde, utaskia uchungu kidogo.

6. **MITUMBA:** Kama nimenusurika risasi, sitakufa hivi karibuni.

7. **SFX: HERBS BEING RUBBED INTO A WOUND**

8. **MITUMBA:** **(screams in agony)** Arrrrrrrgh!!!! Lela, unataka kuniua? Umekuwa hao watorube huko nje?

**(Both Lela and Shani react shockingly)**

9. **LELA:** Haiwezekani! Kivipi watorube ndio wanatupiga risasi ? Kwanini?

**10. SHANI:** Baba, kweli una hakika? Labda bado uko kwenye mshtuko, na hukumbuki ulichoona.

**11. MITUMBA:** Hata kama mimi ni mzee, lakini sio hivyo. Najua nimeona nini huko nje. Wanaume wote na hata vijana wadogo wakitorube walnafyetuwa risasi. Gulu, kijana wa Masomba ndiye aliyenilenga hasa.

**12. SHANI:** **(shocked)** Gulu! Haliwezekani. Kwa nini atake kukuua?

**13. MITUMBA:** Labda ataka nife ndiyo asiweze kulipa mahari.

**(They all laugh but in a controlled way)**

**14. LELA:** Haiwezekani, Gulu alikuwa na sisi shambani, akitusaidia kupanda mbegu siku ile. Na ni juzi tu tulisherehekea maridhiano, uhasama huu wa ghafla umetoka wapi tena?

**15. SFX: KNOCKING ON DOOR**

**16. SHANI:** **(frightened, whispers)** Ndio hao! Wamefika kutumaliza. Mungu wangu tusaidie.

**17. LELA:** Shani nyamaza. Baba, tufanye nini? Ninaogopa.

18. **MITUMBA:** **(coming to a realization)** Inaonekana watorube walitudanganya. Binti zangu, nawataka radhi. Lakini kama ni kutuua, basi waanze na mimi kwanza.

19. **SFX: MORE KNOCKING ON THE DOOR**

20. **MASAMBO:** **(shouting from outside)** Mitumba! Uko ndani?

21. **MITUMBA:** Masambo, tumewafanya nini watu wako? Mbona munataka kutumaliza?

22. **MASAMBO:** **(apologetic)** Nashukuru mababu zetu uko hai! Nilifikiria umekufa!

23. **MITUMBA:** Ndiyo haja yako kubwa hiyo. Umekuja kutimiza lile mwanao Gulu alishindwa kulitimiza. Sivyo?

24. **MASAMBO:** **(Surprised)** Ati! La! Hapana! Nimekuja hapa, kwa sababu Gulu ameniambia kuwa alikupiga risasi kimakosa. Alikuwa anajaaribu bunduki aliyopewa na serikali ilikujikinga na waasi wakimbebe wanaokuja kutuibia ng’ombe.

25. **GULU:** **(sad and apologetic)** Niwie radhi bwana Mitumba, sikunuia kukudhuru. Nilishikwa na fazaiko. Tafadhali nisamehe. Singelitaka kamwe ku…...

**26. SFX: DOOR BEING OPENED**

**27. SHANI:** Nakuamini Gulu.

**28. MITUMBA:** Shani!

**29. MASAMBO:** Tafadhali msamehe mwanangu Mitumba, na kama ni matakwa yako, sijui nikulipe nini? Si unakumbuka sisi ni kama jamii moja sasa.

**30. SHANI:** Msamehe baba, mtazame. Unaona anavyohuzunika, ni ajali iliyotokea.

**31. LELA:** Baba, Shani asema kweli. Ajali humtokea yeyote. Na sasa tumefahamu kuwa hawakuwa na lengo la kutumaliza.

**32. MITUMBA:** Sawa, sawa, Gulu, nakusamehe. Lakini wakati mwengine, tazama unapolenga, ah, hapana lenga kule unapotazama! Ingieni ndani, na muniambie kiini cha serikali kuwapa bunduki?

**33. MASAMBO:** Haujui? Nilifikiri wamempa kila mtu bunduki hapa bonde la Kijani. Hata hivyo huna haja ya kuhofu kitu. Sisi ni marafiki. Ni wale washenzi, makatili wakimbebe watakaolipa kwa ufilisi na uchungu waliotupa.

34. **MSIMULIZI:** Masambo alichukua muda kumueleza Mitumba kuhusu Kero alivyokuja na gari la wanajeshi liliojaa bunduki, kuwagawanyia watorube. Habari hizi hazikushangaza pekee, bali ziliitia hofu familia ya Mitumba. Hawakuelewa kwanini kabila moja pekee lipewe silaha, na mengine yawachwe bila kinga yeyote. Baada ya siku chache, muda wa kulipa kisasi uliwadia. Lawi ndiye aliyekuwa kiongozi wa uvamizi huo, asubui mbichi ya mafungua ng’ombe.

**<u>SCENE TWO: TORUBE ATTACK KIMBEBE IN THEIR TERRITORY</u>**

35. **SFX: MORNING AMBIENCE IN THE VILLAGE**

36. **LAWI:** **(commanding voice, whispering)** Nisikilizeni nyote! Watu tunaotaka kuwavamia sio marafiki zetu. Sio ndugu zetu wala majirani! Wameua marafiki zetu, wameteka nyara watu wetu, wamenajisi dada zetu na kuiba mifugo yetu . Tena mara kwa mara. Leo, turegesheni mali na vitu vyetu vyote walivyotupora. Tuletee mama na wazee wetu sababu ya wao kujivinua! **(shouting)** Sawa, tuanze uvamizi - Twendeni!

37. **SFX: FIRING OF GUNS, GRENADES**

38. **(women wailing and children crying)**

39. **SHORT SILENCE**

40. **LAWI:** **(screams)** Torube iyaaah!!

41. **(men respond “iyaah” and start sing victorious war songs: iyaah, iyaah, iyaah…..)**

42. **LAWI:** Wamesalimu amri. Turegesheni ng’ombe zetu nyumbani, wafungeni hao waliosalimu amri, na tuwaregeshe kwa mikono ya serikali. Musiwadhuru wanawake wala watoto! Weweee! Musichome nyumba zao!

43. **SFX: FIRE BLAZING AND RAZING DOWN A STRUCTURE**

44. **LAWI:** **(screaming)** La!!!!!!!! wacheni! wacha!! Usipige risasi!

45. **SFX: MORE FIRING FROM GUNS**

46. **MSIMULIZI:** Lawi alichelewa, uharibifu na mauaji ya kikatili yalishatendeka. Nani wa kulaumiwa kwa kitendo hicho cha kuogofya? Ni yule anayefyetulia risasi watu wasio na hatia wala silaha? Au yule aliyewapa watorube silaha? Ni yule aliyeuza bunduki? Au yule anayeonekana kama adui? Mauaji haya ya kinyama yataendelea hadi lini? Tunapojiuliza haya maswali, Lawi na wenzake waliiongoza mifugo iliyokuwa imechukuliwa na wahalifu hadi nyumbani, wakiacha nyuma maiti nyingi na nyumba zikiwaka moto. Kule jijini, kura ziliwadia. Kura za maoni zilikwenda juu kwa Matonge. Na hii ilimfurahisha yeye na washauri wake wawili, Kero na Somba wakati walipokutana.

## SCENE THREE: MATONGE, SOMBA AND KERO MEET

47. **KERO:** Muheshimiwa Rais, inaonekana twaongoza tena katika kindumbwendumbwe cha kupigania urais! Sikiliza habari zinasemaje..

48. **SFX: NEWSPAPER BEING SHUFFLED**

49. **KERO:** **(reads out)** "Kura za watorube zamponyoka Roselyn na kumwendea Rais ".

50. **MATONGE:** Maridadi. Niambie, Kero ni waasi wangapi wakimbebe waliotekwa na watorube katika vamizi lao?

51. **KERO:** Wengi. Tayari tumewaweka kizuizini mwetu. Lakini kiongozi wao Dere hakuwepo.

52. **MATONGE:** Na wangapi wameuawa, Jenerali Somba?

53. **SOMBA:** Wengi. Lakini hakuna la mswalie. Mambo haya ni ya kawaida sehemu hiyo ya nchi. Muhimu ni kuwa tunashinda huu uchaguzi. Mpango wetu unafaulu.

54. **MATONGE:** Vyema! Tafadhali, jenerali Somba, peleka silaha zaidi kwa watorube. Wananisaidia kuua jiwe moja kwa ndege wawili.

**55. KERO:** **(bursts out laughing)** Umeukosea msemo huo rais. Ni kuua ndege wawili kwa jiwe moja.

**56. MATONGE:** Bora umeelewa na matokeo ni yale yale. Tunawamaliza waasi wakimbebe na kumaliza chama cha upinzani. Kero, shukrani kwa utiifu. Hutaambulia patupu nikishafaulu.

**57. KERO:** Kuna shida kidogo lakini, Mheshimiwa. Wakati wa uvamizi wa waasi wakimbebe , baadhi ya wafanyikazi wa umoja wa mataifa pia waliuawa, wale waliobakia hai wanasema huu ulikuwa ni uuaji watu bila hatia, na wameuita utawala wako, utawala wa kidikteta.

**58. MATONGE:** Uuaji watu bila hatia? Hawa wageni wanashida gani? Watu wangu wanavamiwa kila uchao, wanapoteza mifugo yao kila siku. Vamizi moja la kulipa kisasi linaitwa mauaji bila hatia? Umeyasikia wapi hayo, Kero?

**59. KERO:** Yamekuwa matangazo yakurudiwa kila wakati katika matoleo ya habari za kimataifa, lakini hapa nimezifunika. Nafikiri kuna haja ya kujisafisha jina, toa taarifa ya umma na ukemee uuaji na kuzihuzunikia tanzia za wafu hao. Hili ni muhimu kwako kama mtu wa watu nchini.

**60. MATONGE:** Kero, una hekima kushinda wazee mia moja. Nitayarishie hotuba ya Rais kuhusu hayo.

**61. KERO:** Bila kupoteza wakati, mheshimiwa rais. Usisahau kusema utatoa msamaha kwa wale waasi watakaosalimu amri. Unachotaka ni amani.

**62. MATONGE:** Hiyo si uongo, kwamba sitaki amani ? Ni vile wakati mwengine, inapatikana kwa damu.

**OUTRO:**

Maneno aliyotamka Rais hapo mwisho yana ukweli. Sote tunahitaji kuishi pamoja kwa amani, hususan kwa mataifa yaliojaa ghasia barani Afrika. Afrika imeenea makundi haramu yaliyo na silaha. Kuanzia magharibi hadi mashariki, kusini, kaskazini hata na ya kati, hakuna sehemu ya bara Afrika ambayo haijawahi kukumbwa na mikinzano. Lakini utatuzi ni upi katika mkinzano huu? Jiunge nasi ukitaka majibu ya kipindi hiki. Ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki, au chengine kilichotangulia, au kutupa maoni, tembelea tovuti yetu www.dw-world.de/lbe. Kwaheri kwa sasa.